# Ujenzi wa Ujitambuzinafsi Hasi katika Bunilizi za *Omar Babu*

*Kawira Kamwara, Kineene wa Mutiso na Amiri Swaleh*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Ujenzi wa ujitambuzinafsi ni suala–ambalo limeshughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili kiutunzi au kiutafiti. Suala hili hujitokeza kupitia kwa jinsi watunzi wa kazi za sanaa wanavyowasawiri wahusika kwa minajili ya kukuza maudhui. Usawiri wa wahusika huathiriwa na itikadi za jamii lengwa zikiwemo utamaduni hasi unaotia nguvu mfumo wa ki-ubabedume ambao umechangia pakubwa ujenzi wa ujitambuzinafsi huu. Hata hivyo, kwa kiwango fulani mwanamke mwenyewe amechangia hali hii kwa kujidunisha mwenyewe au kwa kukosa sauti na ujasiri wa kusimama kidete na kujiamulia mustakabali wake. Suala hili limejitokeza katika bunilizi za Omar Babu ambazo ni *Kala Tufaha* (2007*),* hadithi fupi ya 'Ndoa ya Samani' katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2010) na *Heri Subira* (2010). Katika bunilizi teule, mwandishi ameliangazia suala la ujenzi wa ujitambuzinafsi hasi wa jinsia ya kike kwa kiwango kikubwa. Ingawa mwandishi huyu anapania kujenga sauti ya mwanamke katika jamii iliyombana na mila zilizopitwa na wakati, katika makala hii tumelengakuonyesha na kutathmini namna ambavyo Babu amewasawiri wahusika wake ili kubainisha hali halisi ya mwanamke katika jamii husika. Uchanganuzi wetu umeongozwa na Ufeministi wa Kiafrika ambao ni mojawapo wa matapo ya Nadharia ya Ufeministi. Utamaduni unampa mwanamke nafasi gani katika jamii? Ni ipi taswira ya uhusiano wa mwanaume na mwanamke katika jamii ya Kiafrika? Je, mwanamke amechangia kwa njia gani hali yake? Tunapania kuyajibu maswali haya katika Makala haya.**

**Maneno Muhimu**: Bunilizi, Ujenzi, Upembezwaji, Ujitambuzinafsi

## Utangulizi

Ujitambuzinafsi ni suala ambalo limewashughulisha watunzi, wasomi na watafiti katika nyanja nyingi za kiusomi wanaotafiti masuala ya mitagusano ya kijamii, mipangilio ya kijamii na mahusiano ya kijinsia miongoni mwa makundi ya kijamii. Kwa upande mmoja, linahusishwa na uwepo wa tungo za kifasihi katika tanzu zote ambapo inaweza kuonyeshwa kwamba, masuala ya mwanamke kupembezwa yanajitokeza. Iwe suala la upembezwaji wa wanawake wa aina yoyote ile linashughulikiwa kiutunzi au kiutafiti, kuna ukweli usiokanika kwamba, linachipuka kutokana na uhalisi wa mitagusano na maingiliano ya kijamii katika misingi ya kijinsia. Kauli hii inaakisika katika usemi wa Wamitila

(2002) kwamba, fasihi ni kioo cha jamii kinachowezesha kuangaziwa kwa hali halisi ya maisha katika jamii husika.

Kimsingi, usawiri wa mwanamke huakisi hali halisi ya mwanamke katika jamii kama anavyobaini Chesaina (1987), anapohakiki jukumu na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia zilizoandikwa kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. Tamthilia za Kiswahili alizohakiki ni Muhando (1972) *Hatia*, Ngozi (1977) *Machozi ya Mwanamke* na Muhando (1982) *Nguzo Mama*. Kimsingi, mtafiti huyu anahoji kwamba, tamthilia kama sanaa halisi ya kiutendaji ni kielelezo bora cha usawiri hasi wa mitazamo na misimamo ya mwanamume pamoja na udhalimu wake dhidi ya mwanamke. Kauli inayoweza kuhusishwa na tafiti za Chesaina ni kwamba, vita dhidi ya mfumo wa ki-ubabedume ni vita batili, havina fanaka kwa kuwa vinatekelezwa katika miktadha na kwa mitazamo ya ki-ubabedume.

Ndung'o (1998) anaangazia mielekeo ya kijamii kuhusu ujitambuzinafsi wa jinsia. Anasema kuwa mila na desturi ni baadhi ya vigezo vinavyosimamisha jamii kama asasi muhimu kupitia kanuni za kijinsia  kupitia kwa fasihi simulizi. Hivyo basi, kupitia kwa methali teule za Wakikuyu na Waswahili, inabainika kuwa mwanamke amejengewa ujitambuzinafsi hasi. Hoja hii hutegemea miktadha ya matumizi ya methali husika. Kwa mujibu wa mila na desturi za jamii za Kiafrika, mwanamume anahusishwa na hekima ya kuielekeza jamii na hivyo, kumjengea ujitambuzinafsi chanya huku mwanamke akidunishwa.

Mavisi (2011) anahakiki riwaya tatu za Burhani ambazo ni *Mali ya Masikini* (1981), *Mwisho wa Kosa* (1987) na *Kipimo cha Mizani* (2004) na kuhoji kuwa mwanamke barani Afrika, anajengewa ujitambuzinafsi hasi tangu utotoni. Kupitia kwa malezi, mvulana hukua akionyeshwa kuwa yeye ni tofauti na msichana na kutengewa majikumu kijinsia. Mtazamo kama huu humwathiri mtoto wa kike kwani, humfanya mtoto wa kiume kujichukulia kuwa bora kuliko mtoto wa kike. Hivyo basi, binadamu wote wanatakiwa kupewa nafasi sawa katika ujenzi wa jamii. Mavisi anapinga kauli kuwa, jukumu la mwanamke ni malezi kwani anaweza kunawiri kielimu.

Uhakiki huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hili ni tawi moja la nadharia ya Ufeministi ambayo huangazia masuala ya kijinsia katika jamii. Ni nadharia iliyoasisiwa na Wollstonecraft (1792) katika makala yake yaliyotetea ujenzi wa ujitambuzinafsi wa jamii usiowabagua wanajamii kwa misingi ya jinsia. Nadharia hi inaungwa mkono na Beauvoir (1949), katika kupinga kila aina za dhuluma za kijinsia. Kulingana na nadharia hii, hakuna tofauti kati ya jinsia ya kike na ya kiume isipokuwa tu za kimaumbile. Hupinga mfumojamii unaojenga ujitambuzinafsi hasi wa jinsia kisiasa, kisheria na kidini. Kwa kupitia mtazamo wa Beauvoir, utamaduni unaozingatiwa na jamii una nguvu ya aina fulani inayotumiwa kama kigezo cha kuiongoza.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilizuliwa na Steady mnamo mwaka 1981 ili kuangazia masuala ya kijinsia barani Afrika na hutazama majukumu ya kijinsia kama yanayokamilishana. Huchunguza asasi zinazomthamini na zile zinazompembeza mwanamke na kusababisha madhara kwake. Katika makala yake ya 2005, mwanaharakati huyu anadai kuwa, bado mwanamke anapembezwa mbali na wito wa muda mrefu kutoka kwa wasomi na wanaharakati wa masuala ya jinsia kumpa mwanamke nafasi stahiki katika jamii. Badala yake, mwanamke anazidi kupembezwa kirangi, kijinsia, kikabila, kitabaka pamoja kiitikadi. Steady anapendekeza uundwaji wa sera za kimsingi zitakazoongoza tafiti zaidi ambazo zinalenga kuchunguza na kubainisha ujenzi wa utambuzinafsia wa jinsia katika bunilizi za Babu.

## Mwalimu Selemani kama Ishara ya Ubabedume na Utamaduni Hasi katika *Kala Tufaha (2010)*

Momanyi (1998) anafafanua mfumo wa ki-ubabedume kama utaratibu na kanuni zinazoonyesha kuhalalishwa kwa asasi za kijamii zenye kugawa majukumu kwa msingi wa kijinsia. Ni mfumo unaompa mwanamume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja za kijamii. Hali hii humtwaza mwanamume na kumtweza mwanamke. Katika bunilizi ya '*Kala Tufaha'* (2007), mwandishi ameangazia dhana ya utamaduni na mfumo wa ki-ubabedume kupitia sifa za wahusika wa kiume. Kwa mfano, Mwalimu Selemani anasawiriwa kama mhusika anayeshikilia mtazamo jadi kuhusu mwanamke unamfanya kumnyima bintiye Kibibi nafasi ya kuendeleza elimu. Ingawa Kibibi anaibuka mwanafunzi bora tarafani anakosa karo yake ya shule ya upili. Msimamo wake ni kuwa, mtoto msichana akisoma hupata fursa ya kutagusana na wavulana ambapo matokeo huwa mimba za mapema.

Anayathamini masomo ya mvulana na ndiyo sababu anamtafutia Imu shule ya sekondari ingawa anashika mkia katika darasa lao. Kwa mwalimu Selemani, Imu ni mvulana atakayewafaa wazazi watakapokuwa mbali na Kibibi atakayeolewa na kufaidi ukweni. Mtazamo huu hasi ndio unamfanya kusema, *"Kiasi cha miaka miwili mitatu nataka binti yangu aolewe*," (uk 29). Kwa Mwalimu Selemani, msichana anastahili kuolewa mapema ili mzazi na binti mwenyewe wajiepushe na aibu. Anasema:

> *"Enzi imebadilika," alipenda kusisitiza, "Wanachosoma nini kama si kufundishwa kwenda tupu tupu? Waone na hivyo viatu virefu wanakwenda kwa matao kama tausi. Viatu juu kwa juu utafikiri wananuia kurufai angani! Mavazi ndiyo hayo yanayoonyesha kwingi zaidi ya yanakositiri, kama pazia! La hasa! Mwanangu kamwe h'endi katika hizo shule." (uk 18).*

Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii yake, msichana anastahili kuvalia 'mufti'. Mafundisho ya kidini ya Mwalimu Selemani yanasisitiza msichana avae

buibui na hijabu akitarajia kuonyesha urembo wake kwa mume atakayemwoa. Mwanamke amewekewa kaida kuhusu hali ya kutembea, mavazi tena hata maongezi. Mwalimu Selemani anachukua nafasi yake kama kiongozi wa familia kutoa kauli kuhusu maisha ya bintiye. Anapendelea maoni yake yazingatiwe bila swali lolote lile. Msimamo wake unadhihirisha ubinafsi na taasubi za kiume kumhusu mwanamke. Sio kwamba hana uwezo wa kumsomesha bintiye, ila tu ni kumkatizia masomo asije akafaidi ukweni baada ya kuhitimisha masomo. Mwalimu Selemani anampembeza mwanamke na kumjengea utambuzinafsi hasi kwa kumchukulia kama chombo cha kuozwa ili yeye babake, afaidi mahari. Hampi mwanamke nafasi ya kujiendeleza kielimu na kushiriki kikamilifu katika nyanja za kiuchumi na kielimu.

Tumetaja kuwa, kusudi la Mwalimu Selemani ni kumwoza Kibibi kisirisiri; lakini Kibibi anabakwa na mwajiri wake. Anaporudi kwao nyumbani, babake anamtelekeza na kumwambia asiwahi kufika nyumbani kwao. Aibu aliyohofia kumfika, ilikuwa imemfikia. Taasubi ya kiume ya Fumbwe inamfanya Kibibi ahangaike bila makao. Babake Mwalimu Selemani, anakaulisha kwa kusema,

> "*Sitaki kabisa kukuona kwangu. Izara uliyotushushia inatutosha. Nasema nyumba yangu hii uione paa na moshi... nikikupata nikirudi, mauti yanakuita*!" (uk.91).

Kupitia usawiri na ujenzi wa ujitambuzinafsi hasi wa mwanamke, Mwalimu Selemani hataki kuchunguza kilichomsababishia Kibibi ujauzito. Kibibi anapojaribu kufafanua kadhia yake, babake hamsikilizi ila anamhukumu kupitia buibui pana alilovalia, mapambo na hulka yake kwa jumla. Badala ya kumchukulia Fumbwe hatua, Kibibi analaumiwa na kuambiwa kuwa ni yeye binafsi ndiye alisababisha tukio la kubakwa. Inasikitisha kuona jinsi mwanamke anavyonyimwa haki na kuhukumiwa kwa makosa yasiyo yake. Mzee Selemani anamjengea Kibibi utambuzinafsi hasi kwa kumchukulia kama mtovu wa nidhamu ilhali yanayomtendea ni kinyume na matarajio yake. Babu anaikashifu jamii hii kwa kutumia vigezo na mizani mbili tofauti katika kuwahukumu wanawake na wanaume.

### Kibibi kama Mhasiriwa wa Ujitambuzinafsi hasi wa Jinsia ya Kike

Katika bunilizi ya *Kala Tufaha* (2010) mwandishi anamtumia Kibibi kuonesha jinsi nyingi za Kiafrika humbagua mwanamke kumfanya ajijengee ujitambuzinafsia hasi. Hoja hii inaungwa mkono na mwanaufeministi Beauvoir (1949) anaposema kuwa, mwanamke wa Kiafrika amefungwa na pingu za utamaduni na kufanya kukubali kila aina ya upembezwaji dhidi yake. Pindi mwanamke anapokubali kupembezwa, utamaduni hutumiwa kama chombo cha kueneza mila na desturi zinazomdhalalisha mwanamke na kumjengea ujitambuzinafsi hasi wa jinsia yake.

Babake Kibibi, Mwalimu Selemani, anakataa kugharamia masomo yake ya shule ya upili kwa kuchukulia kwamba, kumwelimisha mtoto-msichana ni kama njia moja ya kumfundisha tabia zilizo kinyume na za jamii yake:

> *"Unadhani nitabadili msimamo wangu? Mimi sitaki kuukaribisha ukahaba nyumbani kwangu! Mwangalie Chaurembo bintiye Mosi. Alipokwenda kusoma jijini alifika wapi? Alirudi nyumbani na digrii gani? Shahada yake ilikuwa mtoto wa kiume! Sitaki aibu…" (uk. 30)*

Tunaweza kusema kuwa, imani ya jadi inamfanya Mwalimu Selemani kukisia kwamba, iwapo mtoto msichana angepata masomo ya sekondari, angeharibika tena akiuke maadili aliyofunza na kuyarithi kutoka kwa wazazi wake. Mwalimu Selemani ana uhuru, mamlaka na uwezo kutokana na itikadi ya jamii yake ya kumwoza Kibibi mapema ili kuepuka "aibu". Msimamo jadi wa Mwalimu Selemani kumhusu mwanamke unamjengea bintiye ujitambuzinafsi hasi kwa kumnyima nafasi ya kupata elimu na kujisimamia kiuchumi. Mwalimu Selemani anakiangamiza kizazi cha baadaye kwa kukinyima nafasi ya kushika hatamu katika maendeleo.

Kupitia kwa mhusika Kibibi, Babu anaonyesha jinsi mwanamke anakosa kujielewa na kupigania anachokithamini. Hali hii inamfanya kukosa ukombozi wake anaoupania. Kibibi anakata tamaa ya kuendelea na masomo. Hatafuti msaada kwa wafadhili au serikali. Anaridhishwa na masomo ya shule ya msingi na kusema;

> *"pengine afadhali mimi. Mamangu kaacha masomo darasa la tatu akaja kuolewa. Bibi zangu kuumeni na kuukeni, hawakulikurubia jengo la shule"* (Uk. 22).. Anakosa kutambua kwamba, ana uwezo wa kushiriki katika maendeleo ya jamii sawa na mwanaume. Mwanamke anaposhindwa kujinasua kutoka mikononi mwa utamaduni kandamizi, hutamauka na kukosa kukimbilia ndoto zake.

**Fumbwe kama Ishara ya Ujenzi wa Ujitambuzinafsi hasi wa Jinsia ya Kike**

Jamii za Kiafrika zinazozingatia mfumo wa ki-ubabedume, humfanya mwamume kujenga fikra kwamba, yeye ni bora kuliko mwanamke. Mwanamume hutumia nguvu na mamlaka anayopewa na jamii kumkandamiza mwamake na kumfanya chombo cha kutimiza uchu wake wa kimapenzi. Jambo hili linapotendeka, mwanamke huachwa na jeraha ambalo haliponi hadi kufa kwake. Katika hadithi ya *Kala Tufaha* (2007), mwandishi anabainisha jinsi mwanamume humjengea mwanamke ujitambuzinafsi hasi katika jamii kupitia kwa mhusika Fumbwe.. Anamdhulumu Kibibi kama tunavyosoma;

> *"… "Huendi kokote!" Binti wa watu alijaribu kijinasua. Fumbwe alikuwa mtu aliyekula akashiba, mwingi wa misuli na kitambi kidogo. Nguvu zake zilitosha kumbeba Kibibi hobelahobela. Kibibi alipata fursa*

*ya kukurupuka na kwenda mlangoni kutaka kutoka. Mara Fumbwe alitoa bastola kwenye mtoto mmoja wa kabati. "Dhubutu na utakula risasi…" (uk. 67-68).*

Fumbwe anamchukulia Kibibi kama kiumbe dhaifu na hivyo anamtumia jinsi apendavyo. Mwandishi anaonyesha kuwa, mwanamke ni kiumbe dhaifu kimaumbile. Udhaifu huu unaonekana kupitia kwa dhuluma anazopitia Kibibi mikononi mwa Fumbwe. Wanaufeministi wanaunga mkono hali ya watunzi wa kazi za sanaa kuangazia changamoto anazopitia mwanamke katika jitihda za kupata haki. Ingawa Kibibi anapigania ujitambuzinafsia chanya, juhudi zake ni finyu. Babu anatujengea taswira ya uwezo alio nao mwanamume wa kumkandamiza mwanamke.

Mbali na hayo, Fumbwe anatumia nguvu zake za kimaumbile na wadhifa wake serikalini kuzuia jitihada za Kibibi kutafuta haki. Tunaona jinsi Kibibi anavyotishiwa kwa bastola pindi anapojaribu kutoka nje. Fumbwe anamfokea; "*… thubutu utakula risasi! …Kibibi alikuja matao ya chini, miguu yake ikinyong'onyea, akajikuta anapiga magoti bila kutarajia*…" (uk. 69). Ni bayana kuwa mwanamke anakomeshwa na mwanamume katika jitihada za kupigania haki yake. Mfumo wa ki-ubabedume unampa Fumbwe uwezo na malaka ya kumkandamiza Kibibi na kumfanya kuhangaika kwa sababu ya makosa yasiyo yake.

Mbali na kutumia taasubi za kiume kwake nyumbani, Fumbwe anamwandama Kibibi kwenye kituo cha polisi kumzuia kupata haki baada ya kumbaka. Tunasoma kuwa, Kibibi anaponafasika kuripoti kwenye kituo cha polisi, anakosa haki kufuatia cheo cha Fumbwe katika idara ya polisi. Kibibi anakosa pahali pengine pa kukimbilia na ndipo anarudi kwa Fumbwe ambaye anamkejeli kwa kumwambia, '*Ulidhani utafika mbali? …hapa Kivukoni hakuna lipitalo nisilolijua* (uk.76). Kupitia Fumbwe, mwandishi anaashiria nguvu na uwezo alio nao mwanamume wa kumkandamiza Kibibi (mwanamke) na kuhakikisha kuwa yeye (mwanamume) asingelichukuliwa hatua yoyote kwa kumdhulumu kingono. Kibibi anatafuta haki kwa mawakili wanawake ili Fumbwe ashurutishwe kumtunza mwana anayemzaa na Kibibi. Badala ya kuwajibika, Fumbwe anawakomesha mawakili wa Kibibi. Anamhonga wakili wa kwanza na kufanya njama ya kutekwa nyara wakili wa pili. Fauka ya hayo, anawatuma wahuni kuteketeza kibanda cha bibi kilichokuwa makao yake. Fumbwe anadhamiria kuangamiza ushahidi wa uchunguzi wa damu ili isibainike ndiye baba asilia wa mtoto wa Kibibi. Lakini wakili wa Kibibi anahakikisha kwamba, Fumbwe hapati nafasi ya kuwahonga polisi na kubatili matokeo (uk 102-103).Hatimaye, Kibibi anapata haki kuashiria ushindi wa wanawake na ujenzi wa ujitambuzinafsi chanya kwa jinsia ya kike.

## Ma' Asha kama Nguzo ya Matumaini ya Mwanamke kujijengea Utambuzinafsi Chanya

Jina halisi la Ma'Asha ni Mwanamgeni. Ni mama wa makamo anayeishi mtaani Pumweni. Anamkuta Kibibi akiwa hoi baada ya jaribio la kuavya mimba, Anajitwika jukumu la kumtunza na kumwelekeza Kibibi baada ya kutelekezwa na aila yake. Ma'Asha anathibitisha kuwa wanawake wanahitaji kuungana kama kundi linalodhulumiwa na kupinga kila aina ya upembezwaji dhidi yao. Steady (1981) anasaili kuwa, ni jukumu la mwanamke wa Kiafrika kujielewa na kufahamu nafasi yake katika jamii. Anapomkuta Kibibi akiwa yu hali mahututi, Ma'Asha anajukumika kumpeleka Kibibi hospitalini na kuhakikisha anapata huduma anayohitaji. Ingawa hamfahamu Kibibi, anamwauni kama binadamu na mwanamke mwenzake anapomkuta amezidiwa. Tunasoma:

> "…Nilikupata barabarani, hali taabani, nikakuleta hapa hospitalini. Nilipata msaada wa wanakijiji wenzangu tulijikusuru hadi yako kufika hapa. Mwenyewe ulikuwa hujitambui. Ilinibidi niwadanganye wauguzi hapa kwamba wewe ni mwanangu ili wakubali kukupokea…" (Uk 11).

Kupitia kwa msaada wake kwa Kibibi, Ma'Asha anawakilisha jamii inayojali maslahi ya kila mmoja. Anamhudumia Kibibi pasi kujali kabila au aila yake. Isitoshe, anawashirikisha wanakijiji katika juhudi za kumpeleka Kibibi hospitalini. Hamhukumu Kibibi ingawa anatambua kuwa alikuwa anajaribu kuavya mimba…*nilipokuokota, ulikuwa umejisare matapishi... siku hizi mimba zinazoaviwa hazihesabiki!* (Uk. 11). Ma'Asha ni nuru ya kuangazia kizazi kichanga. Anahakikisha kuwa Kibibi anapata huduma ili kumwokoa pamoja na mtoto aliyebeba tumboni.

Ma'Asha ni mwanamke ambaye tabia yake inaweza kuigwa na wanawake wengine katika jamii. Kimani na Njogu (2002) wanasema kuwa nadharia ya Ufeministi hudhamiria kuwaelekeza watunzi wa kazi za sanaa kubuni kazi zenye wahusika wanawake wanaoweza kuigwa. Ma'Asha anamjengea mwanamke ujitambuzinafsi chanya hasa kwa kukubali kumtunza Kibibi. Ni kielelezo cha mwanamke anayejitwika mzigo wa malezi kwa jamii. Anampa Kibibi mtaji wa kuanzisha biashara ya uchuuzi wa matunda na ya makaa. Kwa ushauri wa Ma'Asha, biashara ya makaa inanawiri na kumwezesha Kibibi kununua vipande vya ardhi na kupanua chumba walimoishi. Tunasoma:

> "Biashara yenyewe ilimwitika Tufaha. Aliyeanza kwa kuuza mikebe alifikia kiwango cha kurundika magunia nje ya nyumba yao. Kila faida aliyopata aliiwekeza kwenye hiyo biashara. Elimu ya mwanawe iliitegemea. Aidha, alitumia biashara hiyo kukidhi maisha yao pale nyumbani" (uk. 135).

Ma'Asha anamtia moyo Kibibi kuzumbua riziki. Mbali na ushauri wa kibiashara, Ma'Asha anampa Kibibi ushauri nasaha kuhusu ndoa, "*Siwezi*

*kukupeleka kwenye dhiki. Unahitaji mwenzio…*" (uk. 139). Salala anapotamani kumwoa Kibibi, anamwomba Ma'Asha amsaidie kumshawishi. Kibibi analikubali kuolewa kwa masharti ya kutotoka kwa Ma'Asha. Ma'Asha anampangia arusi kwa ushirikiano wa Wanapumueni. Ma'Asha ni kielelezo cha mshauri nasaha ambaye anaibua matumaini kwenye nafsi iliyotamauka. Mbali na hayo, Ma'Asha anajitahidi kumwondolea uchungu na kumjengea Kibibi ujitambuzinafsi chanya kwa kumhimiza kuanza maisha ya familia. Arusi inaandaliwa na wanandoa wanaishi kwa furaha.

Ushauri wa Ma'Asha unampa Kibibi matumaini na kuonyesha kuwa, mwanamke sio kiumbe duni na wala kupata mtoto nje ya ndoa si kumaanisha ya kwamba, mtu hawezi kuolewa…"*Mwanangu, tahadhari na dunia. Dunia hadaa. Fikiria mustakabali wako mapema*…(uk. 109). Kwa kuzingatia ushauri wa Ma'Asha, mkondo wa maisha ya Kibibi unabadilika. Anaweza kujikimu na kupata staha katika jamii. Mwandishi ameweza kubaini kwamba, endapo mwanamke atapata ushauri unaofaa, ajitulize, ajitunze, awajibikie shughuli itakayomkimu kimaisha, inakuwa ni hatua muhimu katika kujijengea ujitambuzinafsi chanya katika jamii inayombagua. Mbali na hayo, imebainika kwamba, ukombozi wa mwanamke, unahitaji mapenzi na ushirikiano baina ya wanawake na wanume wenye maono kuhusu umuhimu wa jinsia mbili kushirikiana katika jamii. Wanawake kwa wanaume wanashika hatamu ya kupigania uhuru na haki za mwanamke kama inavyojitokeza kupitia mhusika Bi. Neema.

**Bi Neema: Tumaini la Wanawake na Ujitambuzinafsi wa Jinsia**

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), Bi Neema ni mwanasheria anayeelewa haki za mwanamke kama zilivyopitishwa na kuratibiwa kwenye katiba. Ni mwanamke anayejitolelea mhanga kuhakikisha kuwa Kibibi anapata haki dhidi ya udhalimu anaotendewa na Fumbwe. Bi Neema ni kielelezo cha nguvu na uwezo walio nao wanawake wanapokula yamini kupigania haki zao. Kama wakili anayetetea haki za mwanamke, Bi Neema anapigania ukombozi wa mwanamke kimawazo na kitabia dhidi ya itikadi na mfumo wa ki-ubabedume. Mtazamo wa Bi Neema unaashiria ari na shauku ya kupinga kila aina ya upembezwaji wa mwanamke katika jamii.

Isitoshe, anamtetea Kibibi dhidi ya ubakaji bila kutaraji malipo yoyoye. Anajitolea kuhakikisha kuwa, mwanamke anapata haki anayostahili. Bi. Neema anatumia nafasi yake kama mtetezi wa mwanamke kuziba mianya yote ambayo Fumbwe angeitumia kuhujumu matokeo ya uchunguzi wa damu. Anafaulu kutumia chembechembe za damu ya Fumbwe na Kala Ulaya ili matokeo yasije uyakasambaratishwa. Fumbwe anahangaika na kusema, "*Umefika wapi? Haikuwezekana kwa nini? Wakili wake? Kwani hamkufanya uchunguzi nyinyi? Ulaya? Sasa iweje*?...(uk. 103). Kauli ya Fumbwe inaashiria kuwa, mwanamke

anapotambua uwezo alio nao, anaweza kupigana na kila aina ya dhuluma na upembezwaji dhidi yake.

Hatimaye, Fumbwe anashindwa kuhujumu ushahidi na ukweli unadhihirika kuwa ndiye baba mzazi wa Kala, mtoto wa Kibibi. Kala anapata nafasi bora ya kurithi mali ya Fumbwe kwani Fumbwe anamtambuliwa rasmi kuwa mwanawe wa damu. Fumbwe anasadiki kuwa ana mwana na Kibibi. Fumbwe anamwambia Kala hospitalini:

> *Ila nina mwana ambaye sikuwa naye… Nilimtelekeza akiwa mkembe…Huyo nimemwachia kila kitu…Huyu mwanangu sijui yuko wapi? Wajua tena mambo ya wanaume. Nilimpata nje ya ndoa. Ibilisi alinifanya nikamdhulumu msichana wa watu. Tokeo lake ni mtoto wa kiume. Mamake anaitwa Kibibi… (uk. 185).*

Fumbwe anamtesa Kibibi lakini, hatimaye Kibibi anafaidi kupitia kwa urithi wa Kala. Mwandishi anamtumia Fumbwe kama funzo kwa wanajamii kuwa, kila mmoja anapaswa kuwajibikia kitendo chake. Fumbwe anatubu ingawa anakosa nafasi ya kukutana na mwana alimyetelekeza tangu utotoni. Wanakutana kisadfa, Fumbwe akiwa hospitalini , katika kitanda cha mauti.

### Malezi na Dini kama Vikwazo kwa Ujitambuzinafsi Chanya wa Jinsia katika *Heri Subira* (2010)

Dini ni mojawapo ya asasi za utamaduni wa jamii. Hutumiwa kufafanua majukumu ya wanajamii hasa kwa msingi wa kijinsia. Katika bunilizi ya *Heri Subira* (2010), tunaona jinsi imani ya dini ya Kiislamu inavyomwathiri mwanamke na kumpa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Mafundisho ya kidini yanampa mwanamume nguvu ya kumtawala mwanamke. Kwa mujibu wa jamii anayolenga Babu katika *Heri Subira*, (2010) utamaduni unampa mwanamke nafasi ya pili huku mwanamume akitwikwa maamlaka juu ya mwanamke. Mtazamo huo ndio unaomfanya Mzee Fauz kumpembeza Sabra pamoja kwa kumpangia ndoa za mapema. Mpango wa ndoa ya mapema unasababishwa na dhana kuwa, Sabra anakuwa mtovu wa nidhamu kwa kuanguka na kumlalia mwanamume. Mafundisho ya dini yanamtaka msichana kudumisha ubikira hadi kuolewa kwake. Kutangamana na wavulana ni jambo lililo kinyume na ada anazowekewa mtoto msichana. Tunasoma,

> *Taswira ya Sabra akiwa amekumbatiwa na mvulana chini barabarani ikamjia. Alisonya kwa sauti, alihisi sio kawaida ya mvulana kumkumbatia msichana kwa hali yoyote ile, hasa vijana wa rika lao. Mbona Sabra awe kwenye kundi lenye wavulana? Dalili ya mvua si ni mawingu? Aliuliza ... (uk. 14).*

Tunaelezwa kuwa, Mzee Fauz mwenyewe ndiye anayesababisha ajali inayowafanya wanafunzi kuangukiana. Kwa bahati mbaya, anayemwangukia

mvulana ni bintiye. Mzee Fauz haamini kuwa kitindamimba wake anaweza kumletea 'aibu' ikiwa dada zake waliomtangulia waliolewa kwa heshima. Hofu ya Sabra kuhusiana na wavulana inamfanya Mzee Fauz kumwendea Fadhil ili kupanga ndoa. Sabra anaozwa kwa Khalid ambaye anampembeza kwa kutowajibikia wajibu na majukumu yake kama mume katika ndoa yao. Kwa kupangiwa ndoa, mwanamke anajengewa ujitambuzinafsi hasi kwani, hapewi nafasi ya kujichagulia mchumba ampendaye.

Ndoa za kupangwa zinakuwa na changamoto kwani wanandoa huenda wakakosa kuelewana. Sabra anasaili, *"Mama, mbona nisijichagulie mwenyewe mume kufu yangu?"* (uk. 21) Kwake Sabra, ni heri kupewa nafasi ya kujichagulia mchumba. Shauku ya kujiamlia atakayemwoa inaonyesha shauku ya vijana ya kujiamulia mambo yao bila ushawishi wa wazazi. Ingawa Sabra anahitaji uhuru wa kimawazo, mafundisho ya dini yanamshurutisha kupata radhi za wazee wake. Hivyo, haendi kinyume na uamuzi wa babake kuhusu maisha yake ya baadaye..

**Sabra kama Mhanga wa Asasi za Dini Na Utamaduni**

Mwanaufeministi Steady (1981) akinukuliwa na Mavisi (2011), anasema kuwa fasihi inahitaji kuwa jukwaa la kuielewa hali ya mwanamke katika jamii inayotawaliwa na ubabedume. Kauli hii inathibitishwa kupitia mhusika Sabra katika *Heri Subira* (2010) kwa kupitia katika hali isiyopendeza wala kuridhisha. Jioni moja, anahusika kwenye ajali ya barabarani inayomfanya kumwangukia mvulana wakiwa njiani kutoka shuleni. Hali ya kumlalia mwanamume inajenga taswira isiyopendeza machoni pa babake. Babake haelewi ni vipi bintiye anavyoweza kuasi mila na desturi za jamii yake na kuingiliana na mwanamume asiye hirimu yake.

Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii husika, mwanamume anajukumika kuiongoza familia yake aonavyo mwafaka. Jambo hili linamfanya Mzee Fauz kuchukua hatua ya 'kuzuia aibu kuingia nyumbani kwake'. Anamwendea kabaila mwenzake na kupanga ndoa ya Sabra bila hata kumjuza. Tunasoma,

> *"Nakuomba, Fadhil, hata na huyu shemeji yangu ayasikie. Nataka kumwoza Sabra. Nitafutieni mtu wa kumsitiri... Nataka wakifunga shule tu aolewe… Lau haitawezekana hivyo, nitamkatizia masomo yake akae nyumbani asubiri mume… Badala ya kuenda mbali, kwa nini tusimposee Khalid hapa kwa Fauz?" (Uk. 15).*

Inabainika kwamba, mwanamke hapewi nafasi ya kujiamulia masuala yanayomhusu katika jamii. Masuala ya ndoa yanashughulikiwa na kiongozi wa familia ambaye ni baba. Mzazi ndiye mwamuzi mkuu wa ni lini na nani anayestahili kumwoa binti yake. Kupitia kwa malezi ya Sabra, hapingi kauli ya kuozwa mapema. Anakubaliana na maamuzi ya babake ili apate baraka na radhi kutoka kwake. Na huenda fikra hii na imani hii ya kidini na kitamaduni, ndiyo

inamlazimisha Sabra akubaliane na maoni ya babake ya kumwoza. Sabra anasema, '*haya ni mambo ya kawaida kwetu sisi'… ikiwa waliotutangulia wameyaweza, sisi tuna upungufu gani hata tushindwe?* (uk 24).

Maneno ya Sabra ni ishara ya jinsi utamaduni na mfumo wa Ki-Ubabedume, ulivyomfanya mwanamke kuamini kila kitu kinarithishwa kutoka kizazi hadi kingine. Ndoa kati ya Khalid na Sabra inatawaliwa na ubinafsi mwingim kwa upande wa Khalid. Ni ndoa ya upande mmoja tangu siku ya arusi; kwa kila namna, Sabra anakosa mapenzi ya mumewe. Mumewe hutokomea kwenda anakojua na kutopatikana nyumbani kwa muda usiozidi saa moja (uk. 41). Kupitia kwa tabia hii, Khalid anamjengea mwanamke ujitambuzinafsi hasi kwa kukosa kuwajibika na kumtimizia mkewe Sabra, utangamano wa mume na mke katika ndoa. Anamwacha Sabra na kwenda kustareheka nje na wanawake wengine.

Mwanamke anatarajiwa kunyenyekea na kumtii mumewe. Kabla ya kuingia kwenye chuo cha ndoa, Sabra anaandaliwa kutimiza wajibu huu muhimu. Ndio maana anajitahidi kumridhisha mumewe bila kumkata kauli. Mamake anamwambia, '*Mume ni kichwa cha nyumba. Hadhari kubishana naye... Mumeo akisema fyata ulimi wako.'* (uk. 44). Kauli ya mamake inaashiria jinsi mwanamke anavyonyimwa uhuru wa mawazo hasa kupinga hoja inayomuuza moyo. Kinyume chake, mwanamume anaruhusiwa kumtawala mwanamke. hii ndiyo sababu wa Khalid kuchelewa kuingia nyumbani. Ingawa tabia hii nikero kwa Sabra, bado jamii inamtaraji avumilie na kudumisha ndoa yake. Mwanamke analazimishwa na utamaduni kuvumilia madhila na upweke katika ndoa dhalimu hali ambayo humnyanyasa na kumjengea ujitambuzinafsi hasi

Mbali na matarajio ya jamii kuhusu mwanamke, lazima ifahamike kuwa mwanamke anajielewa mwenyewe na ana haki ya kujijengea ujitambuzinafsi chanya na kukata pingu za upembezwaji wake. Huu ndio mkondo ambao Sabra anauchukua kwa kuiasi ndoa dhalimu na kukimbilia kwa mlezi wake Bi Baraka. Inabainika kuwa, mwanamke anakinai dhuluma na kutamani kuufurahia uhuru wa kibinadamu. Mwanamke anajikomboa baada ya kugundua uwezo wake wa kupinga kaida pembezaji anazowekewa na jamii kufuatia mfumo wa ki-babadume na itikadi za kidini dhidi yake.

### Khalid kama Ishara ya Kutowajibika kwa Wanaume

Khalid ni mwanawe Mzee Fadhil na Mama Johra. Ni mwanamume wa umri wa makamo anayetumia muda wake mwingi kwenye ulevi. Katika *Heri Subira* (2010), Khalid anasawiriwa kama mwakilishi wa mume asiyewajibikia ndoa. Tunaona akimwacha mkewe wa ndoa na kujiburudisha na wanawake wengine. Anakosa kumridhisha mkewe kindoa jambo ambalo linamuudhi mkewe. Tunasoma:

> *Sabra alidhikika sana na tabia ya Khalid ya kutotulia nyumbani. Alijitahidi kufanya taftishi kujua alikokuwa akichelewa. Uchunguzi wake, hata hivyo, haukuambulia chochote, ulimrejesha kwenye upweke wake (uk. 42).*

Dondoo hili linaonyesha kuwa, Khalid haoni umuhimu wa ndoa. Mtazamo wake unatofautishiana na wa Sabra anayeingia katika ndoa kwa madhumuni kumtunza mumewe kadri alivyofunzwa. Badala yake, Khalid hampi Sabra nafasi ya kutimizia ada ya uke. Analala vilabuni na kumwacha mkewe akimtamani. Sabra anasaili '*Kwa nini unaniacha peke yangu? Kwa nini kanipa upweke huu, habibii?'* (uk. 46). Swali la Sabra linaashiria mwanamke anayeumia ndani kwa ndani. Anajaribu kumrai mumewe kwa unyenyekevu angalau aweze kumwonea imani lakini, Khalid habadili tabia yake.

Mbali na kumwacha pekee, tunaelezwa kuwa Khalid anamchapa kila siku. Badala ya kumtunza, anamchukua kama kiumbe dhaifu. Anamkosea heshima na kumsababishia huzuni. Uhusiano baina yao unayoonyesha jinsi mwanamke anavyonyamazishwa katika jamii. Mwanamume anatumia tofauti za kimaumbile kumdhibiti mwanamke. Khalid anadhihirisha uhafidhina wa kumchukulia mwanamke kama milki ya mwanamume hasa baada ya kulipiwa mahari. Hivyo, mwanamume anapewa haki ya na kujichukulia akiwa bora kuliko mwanamke.

### Biti Baraka kama Tumaini la Mwanamke katika Vita dhidi ya Ujitambuzinafsi Hasi katika Jamii

Biti Baraka amesawiriwa kama daraja la kuvukiwa na Sabra katika jitihada za kujikomboa na kujijengea ujitambuzinafsi chanya. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa, watunzi wa kazi ya sanaa waweze kuwa na wahusika wa kike wanaoweza kuigwa. Binti Baraka anaelewa hali ya mwanamke na kumsaidia kuyaendeleza maisha baada ya kudhalilishwa na kujengewa utambuzinafsi hasi. Sabra anamkimbilia baada kutelekezwa na wazaziwe na wakweze. Anapokosa pa kwenda, anapata hifadhi kwa Biti Baraka. Tunasoma:

> *Bibi, naomba nikae kwako kwa muda kisha niondoke nikahangaike na dunia... Mjukuu wangu, usiwe na shaka, najua hapa siwezi kukuweka kama kwa Fauz, kidogo ninachopata tutakula pamoja (uk. 71).*

Kupitia kwa dondoo hili, tunaweza kusema kuwa mwanamke anamwauni mwanamke mwenzakena kumpa tumaini anapotamaushwa na hali ya maisha. Biti Baraka anamsaidia kuanzisha biashara ambayo inanawiri. Mbali na hayo anamsaidia kupata talaka kutoka kwa Khalid. Sabra anapotaka kuolewa na Heri, Biti Baraka anampa ushauri kuhusu taratibu za kupata talaka Anakashifu hatua ya Sabra kupangiwa ndoa ambayo anadhulumiwa na kunyimwa haki kwa kusaili… '*Kwa nini Fauz kufanya hivyo? Mbona asiingilie kati huyo Khalid alipoanza kukuumiza?'...(uk.71).* Mwandishi anamsawiri kama ishara ya kizazi

kinachopigania ujitambuzinafsi chanya katika jamii. Kupitia kwake, mwanamke anapigania na kupata nafasi stahiki katika jamii.

**Fauz kama Kielelezo cha Taasubi ya Kiume**

Momanyi (1998), anasema kuwa katika jamii za Kiafrika zinazozingatia mfumo wa ki-ubabedume, mwanamke anapewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Jamii inampasa kutii na kunyenyekea kwa bila kukaidi maoni ya mumewe kuhusu familia. Hali hii inamfanya Mzee Fauz kumjengea mwanamke ujitambuzinafsi hasi kwa kuwaoza mabinti zake wakiwa wadogo. Hawapi nafasi ya kuendeleza masomo wala kukomaa kimawazo. Tunasoma:

> *Shufaa na Nasra hawakupata kufika mbali kwenye masomo yao. Mzee Fauz kusema kweli, ni kana kwamba jamaa walisubiri wavunje ungo tu. Hata kabla hawajamaliza masomo, posa zilikuwa zimeanza kumiminika (uk. 17).*

Mzee Fauz ndiye anayeamua masuala ya familia yake. Kama kiongozi wa familia, anafanya maamuzi yanayomdunisha mwanamke yakiwemo ndoa za mapema na za kupangwa Mbali na hayo, anamlazimisha bintiye kuvumilia udhalilishaji katika ndoa. Baada ya kuteswa na mumewe, Sabra anawaendea wazazi wake akidhani kuwa, angepata usaidizi. Ubinafsi na ubabedume wa babake unamfanya kumhukumu kwa kumharibia jina katika jamii. Mzee Fauz anachukua kama heshima kwa mwanawe kuolewa katika familia ya matajiri hivyo, Khalid anapomjengea Sabra ujitambulizinafsi hasi, babake anamtaka avumilie kwa kumkashifu kwa kutoroka kwake. Anamwambia ...' *Kwa vyovyote vile, Khalid ni mume wako. Kwanza ni kosa kubwa sana kuondoka kwako bila kumwarifu…Usiwahi kuja tena huku kutushtakia…* (uk. 53).

Mwanamke anakosa msaada wa baba mzazi kwani mfumo wa kuumeni unamnyanyasa mwanamke na kumlazimisha kuhatarisha maisha yake. Mzee Fauz ni mwakilishi wa kizazi cha jadi kinachompembeza mwanamke na kumlaumu kwa masaibu katika ndoa yake. Ni kama mwanamke ndiye anayehitajiwa kudumisha ndoa yake. Ndiye anayepaswa kuwaita wazazi wake iwapo anakumbana na changamoto katika ndoa. Inabainika kuwa, jamii inachukulia kuteseka kisaikolojia kwa mwanamke kama jambo la kawaida. Analazimishwa kuishi katika ndoa dhalilishi. Hana satua ya masuala ya ndoa, ingawa ndiye yuko kwenye ndoa ile. Utamaduni haumruhusu mwanamke kuasi mumewe. Iwapo anafanya hivyo, anachukuliwa kama mtovu wa maadili. Ndio sababu babake anamfukuza anapomshaki udhalimu wa mumewe. Ada kuhusu ndoa zimempembeza mwanamke na kumjeruhi moyoni. Kama tulivyotaja, Khalid anamdhulumu mkewe kwa kumpiga na kumwambukiza maradhi ya zinaa.

**Utabaka kama Kikwazo dhidi ya Ujenzi Wa Ujitambuzinafsi Chanya katika 'Ndoa Ya Samani'**

Mama Amali ni mzazi wa mchumba wa msimulizi. Ni mama wa familia yenye hadhi na kipato. Tabaka lake ni la juu na hili ndilo jambo linalomfanya kuhisi kwamba, ana nafasi stahiki katika jamii. Mtazamo wake unamjengea mwanamke ujitambuzinafsi hasi na kusambaratisha juhudi zake za kushirikiana na wanajamii wengine na hasa wanyonge. Masaibu anayomsababishia binti yake yanadhihirisha mtazamo wa wanaufeministi kuhusu nafasi anayopewa mwanamke katika jamii. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kwamba, fasihi inafaa itumike kama jukwaa la kueleza hali halisi ya mwanamke. Mwandishi anatueleza kuwa, posa ya kwanza ya msimulizi inakataliwa. Tunasoma:

> *Nilikuwa nimebeba kifurushi kilichokuwa na majani-chai, sukari na marashi. Tulipowasili, mjomba wangu alimweleza baba yake Amali lengo la ujumbe wetu. Baba yake Amali akaingia jikoni kushauriana na mkewe. Punde walitoka jikoni kuja sebuleni. ' Amali hataki kuolewa, …tena sijui kama utaweza mahari '…. (Uk. 86-87).*

Tunaweza kuhoji kwamba, mama yake Amali anamdhalilisha Abu kwa kuwa ni mtu wa tabaka la chini. Anatarajia binti yake aolewe na mvulana wa tabaka la juu kama lao. Anakosa kuelewa kuwa, utajiri sio kiwango cha kupima utu wa mtu. Tunasoma kuwa, baada ya msimulizi kujengewa utambuzinafsi hasi, anatamauka na kukatiza uhusiano dhidi yake na Amali. Anasema; *Nilitamauka kabisa kiasi kwamba tulipokuwa tukirejelea nyumbani, sikusema lolote ... (Uk. 87)* .

Mama Amali anaua kizazi cha baadaye. Anadhihirisha ubinafsi na ubaguzi wa jinsia kwa msingi wa tabaka. Anakataa posa ya msimulizi kwa kuwa alikuwa maskini. Msimamo wake unabainisha jamii inayotawaliwa na tamaa ya kijizidishia mali hasa kupitia kwa kuwaoza mabinti zake. Mwanamke anajengewa utambuzinafsi hasi kwa kulinganisha dhamani yake na mahari. Tunaweza kusema kuwa, bila kulipiwa mahari msichana hawezi akapata ridhaa ya wazazi wake. Dhana hii inamvunja msimulizi moyo.

Baada ya kukataliwa kwa posa yake, msimulizi anaenda Arabuni na kutundiza fedha. Maisha yake yanaboreka na kuinua maisha yake ya aila yake. Anamposa Amali kwa mara ya pili ambapo posa yake inakubaliwa. Kukubalika kwa posa yake, kunaashiria tamaa ya mali na kujinasibisha kwa misingi ya matabaka katika jamii. Mama Amali yuko tayari kujitambulisha na msimulizi kwa kuwa hali yake imeimarika kiuchumi. Maandalizi ya arusi yanafanywa lakini, tunamwona msimulizi akikataa kufunga ndoa na Amali. Inabainikia kuwa siye anayependwa ila mali yake… *Sikumwoa mimi bali ameolewa na mali yangu. … Mimi si yule waliyenikataa kabla sijaenda Arabuni? (uk. 89).*

Mwandishi anamsawiri Mama Amali na tabaka lake kama kikwazo kwa mwanamke anapowania kujijengea ujitambuzinafsi chanya. Kumwekea msimulizi masharti ya mahari ni kizingiti kwa vijana wanapojiandaa kuanza familia zao. Jamii inawataraji vijana kuoa na kuendeleza kizazi cha baadaye. Wazazi ndio wanaopaswa kuwaelekeza watoto katika masuala ya kijamii. Isitoshe, jamii inawataka kuwa kielelezo kwa vijana wanapokua. Mzazi wa kike ndiye hasa anayejukumishwa na jamii kushika hatamu katika malezi ya watoto kwani ndiye mshauri mkuu hasa watoto wa kike. Badala ya mama Amali kuwa kielelezo kwa jamii katika nyanja ya malezi, anaongozwa na tamaa ya mali na utabaka katika kupinga muungano huo wa vijana.

Mwandishi anaonyesha nafasi ya wazazi katika maamuzi ya watoto wao na jinsi utabaka unavyoweza kuuelekeza na kuuathiri kwa njia hasi. Iwapo wazazi watakosa kumakinika, huenda wakawaathiri watoto wao kwa kuwaamrisha na kuwaelekeza katika maswala yote. Wazazi wa Amali wanawakilisha kizazi kipya kinachoamua masuala ya watoto kwenye misingi ya utabaka. Babake Amali anashauriana na mkewe kwanza kuhusu posa ya Abu. Baada ya kushauriana, Mamake Amali ndiye anayetoa kauli ya mwisho kuhusu posa ya bintiye. Badala ya kumridhia bintiye, ndiye anayepinga ndoa hiyo. Inawezekana tukadai kwamba, huyu ni mwanamke anayekuwa kikwazo katika ujenzi wa ujitambuzinafsi chanya katika jamii kwa kumnyima bintiye nafasi ya kuolewa. Fauka ya hayo, tunaweza kusema kwamba, mama Amali anakiuka wito wa mwanaufeministi Steady (1981), anaposema kuwa wanawake wanahitaji kuungana kama kundi moja lenye azma moja ya kupinga kila aina ya upembezwaji dhidi yao na jinsia ya kike kwa jumla. Mwandishi amefaulu kuipenyeza nafsi ya mwanamke na kuonyesha mtazamo hasi unaomkumba hasa anapoongozwa na tamaa ya mali. Hatua anayoweza kuchukua huenda ikatatiza jamii kwa kutamausha kizazi kipya kujiunga na asasi ya ndoa kadri anavyofanya msimulizi. Huenda ikawa hili ni onyo kwamba, tusipime thamani ya binadamu na utu kwa vipimo vya tabaka lao na uwezo wao kiuchumi. Iwapo jamii itashikilia mambo haya, basi si muhali tuuone ujenzi hasi wa ujitambuzinafsi wa jinsia. Hii ni misimamo na dhana iliyopitwa na wakati. Hivyo, jamii inahitajiwa kulenga na kutekeleza mambo yatakayoboresha utangamano bora wa jinsia pasina kuingiza vikwazo vinavyozidisha utengano na uhasama kati ya jinsia za kike na kiume.

## Hitimisho

Makala haya yameonyesha namna mwanamke anajengewa ujitambuzinasfi hasi katika jamii kwa misingi ya kitabaka. Dhana ya udhaifu wa mwanamke imejitokeza kufuatia kupumbuzwa na itikadi, mila, dini, desturi zinazotiwa nguvu na mfumo ki-ubabedume. Hali hii humfanya mwanamke kuamini na kuchukulia kama hali halisi ya mambo. Kupitia mhusika Kibibi katika *Kala Tufaha,* tunaona jinsi anavyokinzwa nguvu na imani pamoja na mtazamo hasi kwa jinsia ya kike

unaomkatizia masomo. Hali sawa na ya Kibibi inamkumba mhusika Sabra katika *Heri Subira* (2010) anapangiwa ndoa ambayo anaikubali ijapo shingo upande. Ndoa yenyewe inakosa kudumu kwa kutowajibika kwa mumewe Khalid. Katika 'Ndoa ya Samani', tumeona jinsi mwanamke anavyopembezwa kupitia kwa utabaka. Posa ya Abu inakataliwa kwa sababu ya uchochole wake. Msimamo wa mwanamume katika jamii unadhihirika kupitiakwa hatua ya msimulizi ya kuvunja uchumba baina yake na Amali. Katika kazi za Babu, tumeona taswira ya udhaifu wa mwanamke kutokana na utamaduni jadi na mfumo wa ki-ubabedume.

## Marejeleo

Babu, O. (2007). *Kala Tufaha*. Nairobi: Oxford Publishers.

Babu, O. (2010). *Heri Subira*. Nairobi: Oxford Publishers.

Bank, O. (1990). *Faces of Feminism: A study of Feminism as a Social Movement*. Basil Blackwell: USA.

Burhani, Z. (1981). *Mali ya Maskini*. Nairobi: Longman Publishers.

Burhani, Z. (1987). *Mwisho wa Kosa*. Nairobi: Longman Publishers.

Burhani, Z. (2004). *Kipimo cha Mizani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Chacha, C.N. (1982). *Mke Mwenza*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Chesaina, C. (1987). "Women in African Drama: Representation and Role". Tasnifu ya Uzamifu University of Leeds. (Haijachapishwa).

De Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex*. London: Pan Books Publishers.

Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism: Woman in Literature*. London: Longhorn Publishers.

Mavisi, R. (2011) "Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Z. Burhani". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Momanyi, C. (2001). *Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili baada ya mwaka wa 2000: Kuyumbisha Uhalisi*. Dar-es Salaam: TUKI.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. Nairobi: East African Publishing House.

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Nairobi: Muwa Publishers.

Ndung'o, C. (1998). "Images of Women as Exemplified in Gikuyu and Swahili Proverbs". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngozi, I. S. (1977). *Machozi ya Mwanamke*. Dar es Salaam: TPH.

Njogu, K. na R. Chimerah (1999). *Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Steady, F. C. (1981). *Reflecting on the Politics of Sisterhood*. New York: African Wordpress.

Wafula, R. M. na K . Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Phoenix Publisher.

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Women.* London: Blackwell Publishers.